# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA MSAJILI WA VYAMA VYA SIASA

# ELIMU KWA UMMA

## SHERIA YA VYAMA VYA SIASA NA KANUNI ZAKE

## YALIYOMO

**Suala** **Ukurasa**

1.0 UTANGULIZI ................................. 1

2.0 SHERIA ZINAZOSIMAMIWA NA OFISI YA MSAJILI WA VYAMA VYA SIASA ....................................................................2

3.0 MAJUKUMU YA OFISI YA MSAJILI WA VYAMA VYA SIASA.......................... 3

4.0 MAJUKUMU YA OFISI YA MSAJILI WA VYAMA VYA SIASA KATIKA UCHAGUZI MKUU ..........................4

5.0 HAKI NA WAJIBU WA CHAMA CHA SIASA KATIKA UCHAGUZI MKUU ....................................................................6

6.0 VITENDO VINAVYOKATAZWA KWA VYAMA VYA SIASA.......................... 9

7.0 HITIMISHO .................................... 11

(iv) Uvumilivu wa kisiasa; na

(v) Amani, Utulivu, Uzalendo, Muungano wa Tanzania na Umoja wa Kitaifa uliopo kati ka nchi yetu.



# 1.0 UTANGULIZI

Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ni Idara ya Serikali inayojitegemea ambayo ipo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Ofisi hii imeanzishwa mara baada ya kurejeshwa kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa nchini kwa Sheria ya Vyama vya Siasa Sura ya 258. Majukumu ya Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ni kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Vyama vya Siasa na Sheria ya Gharama za Uchaguzi Sura ya 278 ambayo hutumika katika Uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wabunge na Madiwani.

## 2.0 SHERIA ZINAZOSIMAMIWA NA OFISI YA MSAJILI WA VYAMA VYA SIASA

Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa inasimamia utekelezaji wa Sheria zifuatazo pamoja na kanuni zake:

(i) Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura ya 258;
(ii) Sheria ya Gharama za Uchaguzi, Sura ya 278;
(iii) Kanuni za Usajili wa Vyama vya Siasa za Mwaka 2019;
(iv) Kanuni za Maadili ya Vyama vya Siasa za Mwaka 2019;
(v) Kanuni za Baraza la Vyama vya Siasa za Mwaka 2019;
(vi) Kanuni za Fedha za Vyama vya Siasa za Mwaka 2019; na
(vii) Kanuni za Gharama za Uchaguzi za Mwaka 2010.



Serikali au Umma (Kifungu cha 11C(3) na 12(2));
(ix) Kutoa matamshi, kuandaa machapisho, kuharibu au kufanya kitendo chochote chenye dhamira ya kudhalilisha au kudhihaki bendera ya chama kingine (Kifungu cha 11C(5); na
(x) Kufanya mikutano au maandamano bila kufuata utaratibu wa kisheria (Kifungu cha 11).

## 7.0 HITIMISHO

Katika kipindi hiki cha uchaguzi, Msajili anaviasa vyama vyote vya siasa kuzingatia Sheria za Nchi zikiwemo Sheria za Uchaguzi pamoja na Sheria ya Gharama za Uchaguzi, Sheria ya Vyama vya Siasa pamoja na Kanuni zake ili kudumisha mambo yafuatayo:

(i) Ushiriki wa uchaguzi ambao ni jukumu la msingi la chama cha siasa;
(ii) Uhusiano mzuri baina ya wadau;
(iii) Utii wa Sheria bila shuruti;

vikosi vingine vya ulinzi na usalama wa nchi (Kifungu cha 8E(1));

(iii) Kuratibu, kuendesha au kufadhili mafunzo yoyote ya kutumia nguvu au silaha kwa wanachama wake au kwa mtu yeyote (Kifungu cha 8E(2));

(iv) Kuhamasisha udini, ukabila na ukanda (Kifungu cha 9(2)(a));

(v) Kuhamasisha kuvunjika kwa Muungano wa Tanzania au kuwa na lengo la kufanya siasa upande mmoja wa muungano (Kifungu cha 9(2)(b)(d));

(vi) Kuruhusu au kuhamasisha matumizi ya nguvu kama njia ya kufikia malengo ya kisiasa (Kifungu cha 9(2)(c));

(vii) Kuruhusu viongozi au wanachama wake kutumia maneno ya matusi, dhihaka, kashfa na uchochezi, yanayoweza kusababisha uvunjifu wa amani(Kifungu cha 9(2)(f));

(viii) Kupeperusha bendera ya chama, kufanya siasa au kufungua tawi katika maeneo ya kazi, shule, vyuo, ibada, majengo ya



## 3.0 MAJUKUMU YA OFISI YA MSAJILI WA VYAMA VYA SIASA

Majukumu ya Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa yameainishwa katika Sheria ya Vyama vya Siasa (Kifungu cha 4(5)) kama ifuatavyo:

(i) Kusajili Vyama vya Siasa;

(ii) Kufuatilia mchakato wa uteuzi na uchaguzi ndani ya Vyama vya Siasa;

(iii) Kuratibu shughuli za Baraza la Vyama vya Siasa;

(iv) Kufuatilia mapato na matumizi ya Vyama vya Siasa;

(v) Kugawa na kufuatilia matumizi ya fedha za ruzuku kwa Vyama vya Siasa vyenye sifa ya kupata ruzuku;

(vi) Kutoa elimu ya uraia kuhusu sheria zinazosimamiwa na Ofisi ya Msajili wa Vya ma vya Siasa na mfumo wa demokrasia ya vyama vyingi vya siasa;

(vii) Kuratibu elimu ya uraia inayotolewa kwa Vyama vya Siasa;

(viii) Kusimamia utekelezaji wa kanuni za maadili ya Vyama vya Siasa;

(ix) Kuishauri Serikali kuhusu masuala yanayohusu Vyama vya Siasa;

(x) Kuwa kiungo cha mawasiliano kati ya Vyama vya Siasa na Serikali;

(xi) Kufanya tafiti kuhusu Vyama vya Siasa, demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa na masuala ya fedha za Vyama vya Siasa; na

(xii) Kutekeleza jukumu lolote chini ya Sheria hii au Sheria zingine za nchi

## 4.0 MAJUKUMU YA OFISI YA MSAJILI WA VYAMA VYA SIASA KATIKA UCHAGUZI

(i) Kutoa elimu kwa umma kuhusu Sheria ya Vyama vya Siasa na kanuni zake (Kifungu 4(5)(e));

(ii) Kuratibu elimu ya uraia inayotolewa kwa Vyama vya Siasa (Kifungu cha 5A);

(iii) Kufuatilia uteuzi wa wagombea ndani ya Vyama vya Siasa (Kifungu cha 4(5)(b));



taarifa ya mapato na matumizi ya chama (Kifungu cha 13 na Kifungu cha 15(1));

(xi) Kuwasilisha kwa Msajili Ilani ya uchaguzi (Kanuni ya 20 ya Kanuni za Usajili na Ufuatiliaji);

(xii) Kuwasilisha kwa Msajili taarifa kuhusu jambo lolote linalohusu utekelezaji wa Sheria ya Vyama vya Siasa (Kifungu cha 5(b)(1)).

## 6.0 VITENDO VINAVYOKATAZWA KWA VYAMA VYA SIASA

Katika kipindi cha uchaguzi, chama cha siasa hakipaswi kufanya yafuatayo:-

(i) Kunadi sera zinazopingana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Katiba ya Zanzibar na Sheria zingine za nchi (Kifungu cha 6A(1));

(ii) Kuunda kikundi cha ulinzi na usalama cha aina yoyote au kuwa na taasisi inayolenga kufanya majukumu ya Jeshi la Polisi au

(ii) Kulaani, kuepuka na kuchukua hatua zinazofaa kwa mujibu wa Sheria ili kuepusha vitendo vya vurugu, kutumia nguvu, matumizi ya lugha za matusi, kashfa, uchochezi au vitendo vingine vyovyote vinavyoweza kusababisha uvunjifu wa amani (Kifungu cha 9(2)(f)) cha Sheria ya Vyama vya Siasa;

(iii) Kutotoa maneno au maandishi ya uongo dhidi ya mtu au chama kingine cha siasa;

(iv) Kujiepusha na vitendo vyote vya rushwa;

(v) Kujiepusha na vitendo vya udanganyifu;

(vi) Kuwa na uzalendo na kuheshimu mila, desturi na maadili ya taifa letu;

(vii) Kuunga mkono juhudi za Serikali katika masuala yenye maslahi ya kitaifa;

(viii) Kuheshimu viongozi wa nchi na kushindana kwa sera na sio masuala binafsi;

(ix) Kuheshimu misingi ya demokrasia, kudumisha amani, utulivu na umoja wa taifa letu;

(x) Kufuata Sheria na kanuni za fedha na kutoa



(iv) Kusimamia masharti ya Sheria ya Vyama vya Siasa yanayohusika katika uchaguzi (Kifungu cha 4(5)(a));

(v) Kusimamia utekelezaji wa Kanuni za Maadili ya Vyama vya Siasa (Kifungu cha 22(2)(i));

(vi) Kuishauri Serikali kuhusu masuala yanayohusu Vyama vya Siasa (Kifungu cha 4(5)(g));

(vii) Kuwa kiungo kati ya Serikali na Vyama vya Siasa kupitia njia mbalimbali ikiwamo Baraza la Vyama vya Siasa (Kifungu cha 4(5)(h)); na

(viii) Kufuatilia mapato na matumizi ya Vyama vya Siasa (Kifungu cha 4(5)(d)).

## 5.0 HAKI NA WAJIBU WA CHAMA CHA SIASA KATIKA UCHAGUZI

### 5.1 Haki za Chama cha Siasa katika Uchaguzi:-

Chama cha Siasa kina haki zifuatazo:

(i) Kutafuta wanachama na kuungwa mkono na wapiga kura;
(ii) Kuteua wagombea;
(iii) Kufanya kampeni;
(iv) Kushirikiana na chama kingine katika shughuli za uchaguzi kwa kufuata utaratibu uliowekwa kwa mujibu wa Sheria;
(v) Kupata ulinzi wa polisi;
(vi) Kumiliki, kutumia na kupeperusha bendera ya chama katika maeneo ambayo hayakatazwi na Sheria ya Vyama vya Siasa;



(vii) Kuwa na vyanzo halali vya mapato vilivyoainishwa katika sheria kwa ajili ya kuendesha shughuli za chama na siasa (Kifungu cha 13(1)(a-e)); na
(viii) Kutoa elimu ya uraia na elimu ya uchaguzi kwa wananchi kwa mujibu wa Sheria.

### 5.2 Wajibu wa Chama cha Siasa:

Chama cha Siasa kina wajibu ufuatao:

(i) Kuendesha na kufanya kazi zake kwa kuzingatia katiba ya Jamhuri ya Muungano, Katiba ya Zanzibar, sheria zingine za nchi, misingi ya demokrasia, utawala bora, jinsia, sera jumuishi na kuepuka ubaguzi wa aina yoyote(Kifungu cha 6A(1)(2));